**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2024

## URAIA NA MAADILI



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2024

## 06 URAIA NA MAADILI

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2024

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ..................................... iv

1.0 UTANGULIZI ..................................... 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KWA KILA SWALI 2

2.1 Swali la 1: Kudumisha Amani ..................................... 2

2.2 Swali la 2: Kuheshimu Jamii ..................................... 11

2.3 Swali la 3: Kuwa Mstahimilivu ..................................... 18

2.4 Swali la 4: Kuheshimu Jamii ..................................... 26

2.5 Swali la 5: Kuwa Mwajibikaji ..................................... 31

2.6 Swali la 6: Kuwa Mwadilifu ..................................... 38

3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI ..................................... 45

4.0 HITIMISHO ..................................... 46

5.0 MAPENDEKEZO ..................................... 46

Kiambatisho: Ulinganifu wa ufaulu kwa wanafunzi katika kila umahiri kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na mwaka 2023 ..................................... 48

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) kwa mwaka 2024 katika somo la Uraia na Maadili. Taarifa hii in lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wakuza mitaala na wadau mbalimbali wa elimu.

Taarifa hii ni tathmini ya kati inayolenga kuonesha mafanikio ya mfumo wa elimu katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia na Maadili kwa wanafunzi wa Darasa la Nne. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika upimaji umekusudia kuonesha maarifa, ujuzi na mwelekeo ambao mfumo huu wa elimu uliweza au haukuweza kuwapa wanafunzi katika somo hili kwa ngazi ya Darasa la III na IV.

Taarifa hii inaonesha sababu za ufaulu mzuri na ufaulu hafifu wa wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) katika somo la Uraia na Maadili. Sababu za ufaulu mzuri ni uelewa mzuri wa umahiri uliopimwa pamoja na uzingatiaji wa matakwa/mahitaji ya maswali. Pia, sababu za wanafunzi kuwa na ufaulu hafifu au wastani ni pamoja na kuandika majibu yasiyoendana na mahitaji ya maswali, na kushindwa kutumia istilahi sahihi za somo katika kujibu maswali.

Ufaulu wa wanafunzi katika Upimaji huu wa SFNA 2024 ni mzuri kwa sababu wanafunzi 1,321,524 (86.35%) walifaulu na wanafunzi 208,937(13.65%) hawakufaulu.

Baraza linatoa shukrani za dhati kwa wadau wote walioshiriki katika kuandaa taarifa hii.

Prof. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) katika somo la Uraia na Maadili ulifanyika Oktoba 2024. Jumla ya wanafunzi 1,633,272 walisajiliwa kufanya upimaji ambapo wanafunzi 1,530,515 walifanya upimaji huo. Ufaulu wa wanafunzi katika somo hili unaonesha kuwa wanafunzi 1,321,524 (86.35%) walifaulu na wanafunzi 208,937 (13.65%) hawakufaulu. Ufaulu huu umeongezeka kwa asilimia 0.83 ikilinganishwa na mwaka 2023 ambapo wanafunzi 1,321,137 (85.52%) walifaulu upimaji huo.

Upimaji wa somo la Uraia na Maadili ulikuwa na jumla ya maswali sita (6) yaliyogawanywa katika Sehemu A na B, yakiwa na jumla ya vipengele 25. Sehemu A ilikuwa na maswali matatu (3) yenye vipengele kumi na tatu (13) vyenye jumla ya alama 26. Sehemu B ilikuwa na maswali matatu (3) yenye vipengele kumi na mbili (12) vyenye jumla ya alama 24. Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kutoka Sehemu A na B. Upimaji ulikuwa na jumla ya alama 50.

Katika Sehemu A, swali la 1 lilikuwa na vipengele vitano (i) - (v) vya kuchagua jibu sahihi ambapo wanafunzi walitakiwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuandika kwenye kisanduku. Swali la 2 lilikuwa na vipengele vinne vya kuoanisha, na liliwataka wanafunzi kuoanisha maelezo kuhusu Alama za Taifa katika Orodha A na Alama za Taifa katika Orodha B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano. Swali la 3 lilikuwa la kujaza nafasi zilizoachwa wazi. Kila kipengele cha swali katika sehemu hii kilikuwa na uzito wa alama 2, hivyo Sehemu A ilikuwa na jumla ya alama 26.

Aidha, katika Sehemu B, swali la 4 lilikuwa na vipengele vitatu vya kukamilisha aya kwa kuandika maneno yanayokosekana katika kipengele (i) - (iv). Swali la 5 lilikuwa la kuchunguza kwa makini picha na kisha kujibu maswali yaliyofuata ambayo yalikuwa na vipengele (a) - (d). Swali la sita 6 lilihusu kusoma kwa makini kifungu cha habari, kisha kujibu vipegele (a – d). Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 24 ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 2.

Taarifa hii inachambua maswali yote sita yaliyotoka katika aina tano za umahiri mkuu kama ilivyobainishwa kwenye Muhtasari ambao ni *Kuheshimu Jamii, Kuwa Mwajibikaji, Kuwa Mstahimilivu, Kuwa mwadilifu* na *Kudumisha Amani*. Uchambuzi huu pia unabainisha idadi au asilimia ya wanafunzi walioweza au walioshindwa kuandika majibu sahihi, na sababu zilizowafanya washindwe kuandika majibu hayo.

Viwango vya ufaulu wa jumla vimegawanywa katika makundi matatu ya ubora wa ufaulu kwa kuzingatia asilimia ya wanafunzi waliofaulu katika swali husika. Kiwango cha ufaulu cha asilimia 0 – 33 ya wanafunzi katika swali kinahesabika kuwa ni hafifu, asilimia 34 – 66 ni wastani na asilimia 67 – 100 ni kiwango kizuri. Viwango vya ufaulu vimewakilishwa na rangi tofauti: nyekundu (ufaulu hafifu), njano (ufaulu wa wastani) na kijani (ufaulu mzuri). Hivyo, ulinganifu wa ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika kila umahiri na maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne 2024, ikilinganishwa na mwaka 2023, umewasilishwa katika Kiambatisho.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KWA KILA SWALI


Sehemu hii inachambua ufaulu wa wanafunzi katika kila swali/ umahiri kwa kuonesha jumla ya wanafunzi waliofanya swali husika na kuelezea ubora wa majibu yao. Pia, viwango vya ufaulu vya wanafunzi katika kila swali vimewekwa katika makundi manne ambayo ni ufaulu mzuri sana, mzuri, wastani na dhaifu. Lengo ni kuonesha kiwango cha utendaji cha wanafunzi katika swali husika kwa kuzingatia mgawanyo wa alama katika kila swali.

### 2.1 Swali la 1: Kudumisha Amani

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kudumisha Amani.* Swali lilikuwa la kuchagua herufi ya jibu sahihi na lilikuwa na vipengele vitano (i) – (v) ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 2. Jumla ya alama kwa swali zima zilikuwa alama 10. Mwanafunzi alitakiwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika

machaguo manne (A – D) kisha kuiandika herufi katika kisanduku kwenye karatasi ya upimaji.

Takwimu zinaonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani, kwa kuwa wanafunzi 867,700 (56.70%) waliofanya swali hili walipata alama 4 mpaka 10. Hata hivyo, wanafunzi wengine 662,812 (43.30%) walikuwa na ufaulu hafifu, kwani walipata alama 0 mpaka 2. Chati Na. 1 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 1.




**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa Wanafunzi katika swali la 1*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 1 umefanyika kama ifuatavyo:

(i) Makabila yapi yanapatikana Tanzania?
- A Wasambaa na Wapare
- B Wasomali na Wakikuyu
- C Wahutu na Wangoni
- D Wamasai na Wakamba

Kipengele hiki cha swali kilitungwa kutoka katika umahiri mahsusi wa *kuchangamana na watu wenye asili tofauti.* Swali lilipima uwezo wa wanafunzi kubaini asili ya makabila mbalimbali nchini Tanzania.

Wanafunzi wenye maarifa ya kutosha walichagua jibu sahihi A, *Wasambaa na Wapare*. Wanafunzi hawa walifahamu kuwa Wasambaa wanapatikana katika mkoa wa Tanga, wilaya ya Lushoto na Wapare wanapatikana mkoa wa Kilimanjaro katika wilaya za Mwanga na Same. Wanafunzi hawa pia walijua kuwa baadhi ya makabila mengine yanayopatikana Tanzania ni pamoja na Wangoni waliopo mkoa wa Ruvuma, Wahehe mkoa wa Iringa, Wanyamwezi mkoa wa Tabora na Wachaga Mkoa wa Kilimanjaro.

Aidha, baadhi ya wanafunzi walishindwa kuelewa makabila yanayopatikana Tanzania, hivyo walichagua kipotoshi B *Wasomali na Wakikuyu*. Wanafunzi hawa walitakiwa kujua kuwa Wasomali wanaishi zaidi nchini Somalia, lakini pia wapo wengi nchini Ethiopia (hasa eneo la mkoa wa Somali) na nchini Kenya (Kaskazini Mashariki). Kabila la Wakikuyu ni moja ya makabila makubwa nchini Kenya. Wanaishi hasa maeneo ya Mlima Kenya kama Nyeri, Murang'a, Kiambu na sehemu za Nairobi. Wakikuyu pia wameenea katika maeneo mengine ya Kenya kutokana na uhamiaji wa ndani.

Baadhi ya wanafunzi waliochagua kipotoshi C, *Wahutu na Wangoni,* hawakufahamu kuwa kipotoshi hicho kimehusisha kabila la Wahutu linalopatikana nchini Burundi. Wanafunzi hao waliochagua kipotoshi C, walidhihirisha kutokuwa na uelewa wa jamii mbalimbali zinazopatikana nchini na asili zao. Wanafunzi waliochagua kipotoshi D, *Wamasai na Wakamba* hawakujua kuwa Wakamba wanapatikana nchini Kenya. Wanafunzi hao wameonesha ukosefu wa maarifa yanayohusiana na jamii zinazochangamana na asili zao.

(ii) Ni nchi zipi zinaunda Jumuiya ya Afrika Mashariki?

A Tanzania, Sudani Kusini, Uganda, Zambia, Burundi na Rwanda

B Uganda, Msumbiji, Kenya, Sudani Kusini na Burundi

C Rwanda, Tanzania, Burundi, Kenya, Sudani Kusini na Uganda

D Tanzania, Sudani Kusini, Rwanda, Burundi, Kenya na Malawi

Swali hili lilitoka katika Umahiri Mahususi wa *Kujenga urafiki Mwema na Mataifa Mengine*. Swali lilipima uelewa wa wanafunzi kuhusu nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wanafunzi wenye maarifa ya kutosha walichagua jibu sahihi C. *Rwanda, Tanzania, Burundi, Kenya, Sudani Kusini na Uganda*. Wanafunzi hawa walikuwa na uelewa kuwa Jumuiya ya awali ya Afrika Mashariki iliundwa mwaka 1967 na kuvunjika mwaka 1977 kutokana na sababu mbalimbali.

Wanafunzi hawa walielewa kuwa Jumuiya Mpya ya Afrika Mashariki iliyoundwa tarehe 30/11/1999 ilianza kazi tarehe 7/7/2000 ikiwa na malengo ya kukuza na kudumisha umoja kwa kuondoa vikwazo vya kiuchumi, kuwa na maendeleo endelevu miongoni mwa nchi wanachama, kudumisha utawala bora na kudumisha umoja na mshikamano miongoni mwa nchi wanachama.  Kwa sasa Jumuiya hii inaundwa na mataifa nane ambayo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Sudani ya kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya watu wa Kongo na Somalia ambayo ilijiunga tarehe 4/3/2024.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi A, *Tanzania, Sudani Kusini, Uganda, Zambia, Burundi na Rwand*a. Wanafunzi hawa walishindwa kutofautisha majirani wa Tanzania na nchi zinazounda jumuiya ya Afrika Mashariki. Walitakiwa kujua kuwa Zambia ni nchi jirani na Tanzania upande wa kusini. Pia, walitakiwa kujua kuwa Tanzania ni mwanachama wa jumuiya nyingine za kikanda za Afrika kama vile Umoja wa Afrika *(AU)* na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC),* pia ni mwanachama wa Jumuiya nyinginezo za kimataifa kama vile Jumuiya ya Madola (*Common Wealth Countries*), Nchi zisizofungamana na upande wowote *(Non Allignment Movement)* na Umoja wa Mataifa (*UN)*.

Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi B, *Uganda, Msumbiji, Kenya, Sudani Kusini na Burundi* pamoja na D, *Tanzania, Sudani Kusini, Rwanda, Burundi, Kenya na Malawi*, walishindwa kutambua

tofauti ya wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi jirani na Tanzania kama vile Zambia, Malawi na Msumbiji ambazo zinapakana na Tanzania upande wa kusini.

(iii) Namna watu wanavyoishi katika taifa fulani hujulikana kama
  A Utalii wa Taifa
  B Mashindano ya kitaifa
  C Utamaduni wa taifa
  D Alama za taifa

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi wa *Kuheshimu tofauti za kiutamaduni na mitazamo miongoni mwa watu wa jamii tofauti*. Swali lililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu dhana ya utamaduni. Wanafunzi wenye uelewa wa kutosha walichagua chaguo sahihi C, *Utamaduni wa Taifa.* Wanafunzi waliochagua jibu sahihi walitambua kuwa *utamaduni* ni jumla ya mambo yote yanayofanyika katika jamii fulani ikijumuisha mila, asili, jadi na desturi. Utamaduni wa taifa hujumuisha mambo mbalimbali kama vile mila, desturi, *Sanaa na ufundi.* Utamaduni wa taifa unaweza kuoneshwa kupitia vitu kama lugha ya taifa, mavazi, ngoma za asili, sherehe kama harusi, misiba, jando na unyago, vyakula na miiko. Vyote hivi vinatoa taswira ya tabia ya jamii husika ambayo ina maanisha utamaduni. Wanafunzi hao walitambua kuwa utamaduni wa taifa ni muhimu sana na una faida nyingi. Baadhi ya faida hizo ni pamoja na kujenga umoja katika nchi, kuleta watu wa makabila tofauti pamoja, unaitambulisha nchi yetu duniani, kwa mfano lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha maarufu duniani na ndiyo lugha ya taifa letu. Pia utamaduni huleta amani na maelewano katika jamii zetu na uzalendo miongoni mwa raia.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua kipotoshi *A, Utalii wa Taifa*, walishindwa kufahamu kwamba utalii wa Taifa ni jumla ya vivutio vyote vilivyopo katika taifa letu, kama vile mbuga za wanyama, mfano: Serengeti, Manyara na Mikumi. Pia, milima mirefu kama vile Kilimanjaro na Meru, mabonde kama vile bonde la Ufa Manyara na bonde la Lushoto, na vyanzo vya maji kama vile Bahari ya Hindi, Ziwa Viktoria, Ziwa Tanganyika lenye kina kirefu

kuliko maziwa yote duniani, na ziwa Nyasa. Vilevile, mabwawa kama vile bwawa la Nyumba ya Mungu, Mtera na kidatu, madini kama vile *Tanzanite* yanayopatikana eneo la Mirerani mkoani Arusha, nchini Tanzania pekee. Hivyo, wageni kutoka ndani na nje ya nchi wanakuja kuvitazama kwa gharama ya kiingilio kilichowekwa na serikali na hivyo kuchangia pato la taifa letu.

Wanafunzi waliochagua kipotoshi B, *Mashindano ya kitaifa,* walishindwa kufahamu kwamba mashindano ya kitaifa ni mashindano yanayorejelea shindano au ushindani ndani ya nchi ambapo watu binafsi, timu au mashirika hushindana kwa lengo mahususi. Mashindano haya yanaweza kuwa ya aina nyingi, kama vile mashindano ya michezo, mashindano ya kitaaluma, au kibiashara na mara nyingi hupangwa ili kukuza vipaji, uvumbuzi na fahari ya kitaifa. Hivyo, si sahihi kwamba mashindano ya kitaifa ni njia mojawapo ya watu kuishi katika taifa fulani.

Wanafunzi waliochagua Kipotoshi D, *Alama za Taifa*, hawakujua kuwa ni vitu vinavyoitambulisha Tanzania miongoni mwa mataifa mengine kama vile Bendera ya Taifa, Mwenge wa Uhuru, Nembo ya Taifa, Fedha ya Taifa, Mnyama wa taifa (Twiga) na wimbo wa Taifa. Hivyo, wanafunzi hao waliochagua kipotoshi D, walishindwa kutambua kwamba alama za taifa ni utambulisho wa Tanzania na sio utamaduni wa taifa.

(iv) Nini kitatokea endapo utandawazi hautatumika vizuri?

A Kutoweka kwa maadili
B Kushuka kwa thamani ya Elimu
C Kuharibika kwa teknolojia
D Kushuka kwa uchumi

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi wa *Kujenga urafiki mwema na mataifa mengine*. Lilipima uelewa wa wanafunzi kuhusu dhana ya Utandawazi. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi, A. *kutoweka kwa maadili,* walikuwa na ufahamu kuwa utandawazi ni mchakato unaohusisha kuongezeka kwa mwingiliano, ushirikiano, utegemezi na uhusiano kati ya jamii moja na jamii nyingine,

mashirika ya kimataifa, Jumuiya za Kimataifa na Asasi za Kiserikali na zisizokuwa za Kiserikali. Wanafunzi hao walitambua moja wapo ya madhara yanayotokana na utandawazi kuwa ni kutoweka kwa maadili ambako kwa sasa kumeathiri vijana wengi, ikiwa ni pamoja na kujihusisha na matendo yasiyofaa katika jamii, kama vile matumizi ya madawa ya kulevya, uvaaji wa nguo zisizo na staha, na kuangalia picha au video zisizo na maadili, kinyume na desturi na tamaduni zetu. Sababu zote hizi hupelekea kushuka kwa maadili katika taifa letu. Pia, wanafunzi hawa walitambua kuwa utandawazi una madhara mengine, kama vile kupanda na kushuka kwa bei za bidhaa, kusambaa kwa magonjwa, ukosefu wa ajira, kuharibika kwa utamaduni wetu na kuwepo kwa matukio ya kigaidi.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua kipotoshi B, *Kushuka kwa thamani ya Elimu,* hawakufahamu kwamba kushuka kwa thamani ya Elimu kunatokana na mambo kama kutotekelezwa vyema kwa sera ya elimu nchini Tanzania, uwekezaji duni katika sekta ya elimu, upungufu wa vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji, kama vile vitabu vya kiada na ziada na mmomonyoko wa maadili kwa wanafunzi. Sababu hizi husababisha athari katika sekta ya elimu na taifa; kwa mfano, kuzalisha wahitimu wasiokuwa na vigezo, maendeleo duni katika nchi na kuwa tegemezi kwa nchi zilizoendelea.

Wanafunzi waliochagua kipotoshi C, *kuharibika kwa teknolojia* walishindwa kutofautisha kuharibika kwa teknolojia na ukosefu wa elimu ya matumizi sahihi ya teknolojia, ilihali utandawazi hukuza teknolojia kwa kiwango kikubwa. Wanafunzi hao walitakiwa kujua kwamba teknolojia imekuwa ni msingi wa shughuli nyingi za kila siku katika maisha ya sasa. Kuharibika kwa teknolojia kutasababisha kuvunjika kwa biashara na uchumi na huleta madhara kwa huduma muhimu kama vile huduma za afya, huduma za kibenki, huduma za mawasiliano na huduma za usafirishaji, jambo ambalo litasababisha kuvurugika kwa maisha ya kila siku. Aidha, teknolojia inaimarisha huduma za afya, kama vile CT-Scan, upandikizaji wa figo na ujenzi wa barabara na reli za kisasa *(SGR*).

Wanafunzi waliochagua kipotoshi D, *Kushuka kwa Uchumi*, walishindwa kujua kuwa kudorora kwa uchumi kunasababishwa na mambo mbalimbali; kwa mfano, utawala mbovu na taasisi dhaifu, mzigo wa madeni, utegemezi wa bidhaa za msingi, miundombinu duni, mfumuko wa bei na kushuka kwa thamani ya fedha, viwango vya chini vya rasilimali watu, vikwazo vya biashara, ukosefu wa vyanzo vingi vya mapato na utegemezi wa misaada kutoka nje. Kwa ujumla, wanafunzi hawa walitakiwa kutambua kwamba kuzorota kwa uchumi siyo matokeo ya utandawazi, na kwamba siyo moja ya athari za utandawazi.

(v) Ni kwa njia zipi Tanzania inashirikiana kiutamaduni na mataifa mengine?

A Elimu, uvuvi na maadili
B Michezo, muziki na filamu
C Michezo, filamu na uvuvi
D Kilimo, muziki na Michezo

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kuheshimu tofauti za kiutamaduni na mitazamo miongoni mwa watu wa jamii tofauti.* Kilipima uelewa wa wanafunzi kubaini njia za kuboresha uhusiano na mataifa mengine. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi B, *Michezo, Muziki na Filamu* walikuwa na uelewa kuwa Tanzania inashirikiana na nchi nyingine kiutamaduni kupitia nyanja kama michezo, muziki na filamu. Walitambua kuwa Tanzania imekuwa ikishiriki mashindano mbalimbali ya michezo inayojumuisha nchi nyingine ulimwenguni kama vile Kenya, Uganda na mataifa mengine ya Ulaya. Wanafunzi hawa walitambua kuwa watanzania wengi hujifunza tamaduni mbalimbali na lugha kama vile Kiingereza, Kifaransa, kiarabu, Kikorea, Kijapani, Kirusi na Kichina. Kupitia lugha hizi, Watanzania wanawasiliana na watu mbalimbali duniani. Pia watu kutoka mataifa mbalimbali hujifunza lugha ya Kiswahili pamoja na utamaduni wa kitanzania.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *Elimu, Uvuvi na Maadili* walishindwa kutofautisha maana ya elimu, uvuvi na maadili. Wanafunzi walipaswa kujua kwamba elimu ni mchakato

wa kupata maarifa, ujuzi, maadili na mitazamo, kupitia mafundisho rasmi au yasiyo rasmi. Vilevile, elimu husaidia watu binafsi kukua kiakili, kijamii, kihisia na kuwatayarisha kwa ajili ya kutumiza majukumu katika jamii. Uvuvi ni shughuli ya kuvua samaki, kwa ajili ya kitoweo, au biashara. Shughuli ya uvuvi inaweza kufanywa kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kutumia ndoana, nyavu, au mitego, na inaweza kufanyika katika maji baridi au maji ya chumvi. Na kwa upande mwingine, maadili yanarejelea kanuni au sheria zinazoongoza tabia kulingana na kile kinachoaminiwa kuwa sawa au kibaya. Maadili mara nyingi hutokana na imani za kitamaduni, kidini na kifalsafa zinazoathiri jinsi watu wanavyoingiliana na kufanya maamuzi ya kimaadili. Hivyo elimu, uvuvi na maadili si njia za kuboresha ushirikiano miongoni mwa watu.

Wanafunzi waliochagua kipotoshi C*, Michezo, Filamu na Uvuvi*, hawakuelewa kwamba kipotoshi hiki kimejumuisha uvuvi ambao siyo sehemu ya njia ya kushirikiana kiutamaduni. Pia, walitakiwa kujua kwamba michezo inarejelea shughuli za kimwili ambayo inahusisha ujuzi, mashindano na mara nyingi huongozwa na sheria zilizowekwa. Inaweza kuchezwa kibinafsi au katika timu na mara nyingi hufanywa kwa tafrija, burudani, au mashindano ya kitaalamu. Mifano ni pamoja na soka, mpira wa kikapu, tenisi, na kuogelea. Filamu ni hadithi za kuona au simulizi ambazo hurekodiwa na kuoneshwa kwenye skrini. Kwa kawaida ni aina ya burudani iliyoundwa kupitia mchanganyiko wa sinema, uigizaji, mwelekeo, uhariri na sauti. Filamu zinaweza kujumuisha aina mbalimbali za muziki, kama vile drama, vichekesho, matukio au hali halisi. Uvuvi ni moja ya shughuli za kiuchumi ambayo haiwezi kuwa njia ambayo kwayo Tanzania inaweza kushirikiana na mataifa mengine kiutamaduni.


Wanafunzi wengine walichagua Kipotoshi D, *Kilimo, Muziki na Michezo.* Wanafunzi hawa walishindwa kutofautisha dhana hizo tatu, kwa maana kwamba kilimo ni shughuli inayohusu kulima, kupanda mazao, na kufuga wanyama kwa ajili ya chakula, nyuzinyuzi na mazao mengine. Kilimo kinabeba jukumu muhimu katika kutoa mambo muhimu kwa maisha ya mwanadamu na

kinasaidia uchumi ulimwenguni kote. Muziki ni sanaa ya kuchanganya sauti au ala ili kuunda nyimbo zinazoelezea hisia, mawazo, au hadithi. Unahusisha aina na tamaduni mbalimbali ukitumika kama burudani na njia ya mawasiliano. Hivyo, kilimo si sehemu ya njia ambazo Tanzania inaweza kushirikiana na mataifa mengine kiutamaduni.

## 2.2 Swali la 2: Kuheshimu Jamii

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *kuheshimu jamii* na katika umahiri mahususi wa *kuipenda Tanzania kwa kuenzi tunu za nchi na asili yake*. Lilipima uelewa wa wanafunzi kuhusu maana na umuhimu wa Alama za Taifa. Swali hili liliwataka wanafunzi kuoanisha maelezo kuhusu Alama za Taifa katika Orodha A na Alama ya Taifa katika Orodha B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri, kwa kuwa wanafunzi 1,135,288 (74.17%) walifaulu. Wanafunzi 473.011 (30.90%) walipata alama 8. Wanafunzi 334,852 (21.88%) walipata alama 6. Wanafunzi 427,425 (21.39%) walipata alama 4**.** Kwa ujumla, wanafunzi 395,224 (25.83%) waliofanya swali hili walifeli, kwa kuwa walipata kati ya alama 0 na 2. Chati Na. 2 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 2.




**Chati Na.2:** *Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 2*

Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuoanisha maelezo kuhusu Alama za Taifa katika **Orodha A** na Alama ya Taifa katika **Orodha B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

| Orodha A | Herufi | Orodha B |
|---|---|---|
| (i) Alama inayowakilisha uhuru na nuru inayoangaza nchi yetu | ( ) | A Bendera ya taifa<br>B Fedha ya taifa |
| (ii) Alama yenye rangi Nne ambazo ni kijani, bluu, nyeusi na manjano | ( ) | C Mwenge wa uhuru<br>D Mnyama wa taifa |
| (iii) Alama inayoonesha picha ya mwanaume upande wa kushoto na mwanamke upande wa kulia | ( ) | E Nembo ya taifa<br>F Wimbo wa taifa |
| (iv) Alama inayoonesha uzalendo kwa taifa letu | ( ) | |

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele

Katika Kipengele (i), swali lilimtaka mwanafunzi kuoanisha alama ya taifa kutoka Orodha B inayoendana na maelezo ya Orodha A ya alama ya taifa inayowakilisha uhuru na nuru inayoangaza nchi yetu. Wanafunzi ambao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu alama za taifa walichagua jibu sahihi C, *Mwenge wa Uhuru*. Wanafunzi hawa walikuwa wanaelewa kuwa Mwenge wa Uhuru ni alama ya taifa ambayo inaashiria uhuru, amani na umoja. Pia, Mwenge wa Uhuru uliwashwa kwa mara ya kwanza kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro mnamo Desemba 9, 1961. Uliashiria kuangaza nchi na kuvuka mipaka pia kuleta matumaini pasipo kukata tamaa, upendo palipo uadui na heshima palipo dharau. Mbio za Mwenge wa Uhuru hufanyika kila mwaka katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Mwenge wa Uhuru unafaida zifuatazo: kuhamasisha maendeleo ya jamii, kuelimisha jamii, kuchochea uzalendo, kuimarisha amani na umoja, na ufuatiliaji wa miradi ya kiserikali. Kwa ujumla, Mwenge wa Uhuru ni chombo chenye nafasi kubwa katika kujenga na kudumisha misingi ya taifa la Tanzania.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliooanisha na kipotoshi A, *Bendera ya taifa*, walipaswa kuelewa kuwa Bendera ya Taifa ni alama ya uhuru na utambulisho wa taifa, inaashiria umoja na mshikamano kwa watanzania wote, na kufanikisha uzalendo. Pia, ni kipande maalumu cha nguo chenye rangi nne ambazo ni nyeusi, bluu, kijani na manjano. Rangi hizi zina maana kwa taifa letu. Rangi ya kijani inawakilisha uoto wa asili, misitu na mbuga za wanyama. Rangi ya bluu inawakilisha vyanzo vya maji kama vile bahari, maziwa, mito na vijito. Rangi nyeusi inawakilisha watu wa Tanzania. Aidha, rangi ya manjano inawakilisha rasilimali na utajiri wa taifa kama vile madini, gesi asilia na mafuta.

Wanafunzi waliochagua kipotoshi B, *Fedha ya Taifa*, hawakuelewa kuwa fedha ya taifa ni mfumo wa pesa uliokubalika kwa ajili ya matumizi ya kununua na kuuza bidhaa na ulipiaji wa huduma mbalimbali. Walitakiwa kutambua kuwa fedha ya taifa letu inajulikana kama shilingi na ipo katika mfumo wa noti na sarafu.

Fedha ya taifa hutumika kila siku katika jamii zetu kununua bidhaa na kulipia huduma mbalimbali; inasaidia kukuza uchumi wa nchi, ni njia ya kubadilishia bidhaa na huduma na inadhibiti sera za fedha.

Vivyo hivyo, baadhi ya wanafunzi walioanisha na kipotoshi D, *Mnyama wa Taifa (Twiga)* walishindwa kuelewa kuwa mnyama wa taifa letu anaitwa twiga, na anapatikana katika maeneo mbalimbali, kama vile hifadhi za taifa na mbuga za wanyama. Wanafunzi hao walitakiwa kuelewa kwamba twiga ni moja wapo ya wanyama ambao ni kivutio cha utalii katika nchi yetu. Pia, walitakiwa kuelewa kuwa twiga kama mnyama wa taifa anawakilisha na kuonesha uwepo wa wanyama mbalimbali wakuvutia wanaopatikana nchini Tanzania, kama vile tembo, simba na swala.

Vilevile, baadhi ya wanafunzi walioanisha swali hili na kipotoshi E, *Nembo ya Taifa,* walishindwa kuelewa kwamba nembo ya taifa ni muhuri wa serikali unaotumika kuonesha mamlaka kamili ya nchi. Nembo hii hujumuisha baadhi ya vitu kama vile mwenge wa uhuru, bendera ya taifa, pembe za ndovu, bibi na bwana, shoka na jembe, ngao na mkuki, kauli mbiu ya taifa, rangi ya njano na nyekundu na kilele cha mlima Kilimanjaro.  Alama zote hizi zinaelezea vitu mbalimbali vinavyopatikana nchini Tanzania. Mwisho, wanafunzi walioanisha swali hili na kipotoshi F, *Wimbo wa Taifa*, walitakiwa kuelewa kuwa wimbo wa taifa unaimbwa wakati wa matukio muhimu na maalum ya taifa letu; kwa mfano, Rais wa nchi anapotaka kulihutubia taifa au wakati Raisi anapozuru nchi nyingine. Wanafunzi hawa walipaswa kujua kwamba wimbo wa taifa ni sala ya taifa letu la Tanzania na Afrika kwa ujumla.

Kipengele (ii) kilimtaka mwanafunzi kuoanisha alama ya taifa kutoka Orodha B inayoendana na maelezo ya Orodha A ambayo ni alama yenye rangi nne ambazo ni kijani, bluu, nyeusi na manjano. Wanafunzi ambao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu alama za taifa walichagua jibu sahihi A, *Bendera ya Taifa.* Wanafunzi hawa walielewa kuwa Bendera ya Taifa ni alama ya uhuru na utambulisho wa taifa, inaashiria umoja na mshikamano kwa watanzania wote na kufanikisha uzalendo. Bendera ya Taifa ina

rangi nne ambazo ni rangi ya kijani inayowakilisha uoto wa asili, misitu na mbuga za wanyama. Pia, rangi ya bluu inayowakilisha vyanzo vya maji kama vile bahari, maziwa, mito na vijito. Rangi nyeusi inayowakilisha watu wa Tanzania. Kwa kuongezea rangi ya manjano inawakilisha utajiri wa taifa kama vile madini, gesi asilia na mafuta.

Kwa upande mwingine, kuna wanafunzi walioanisha kimakosa swali hili na kipotoshi B, *Fedha ya Taifa.* Wanafunzi hawa walishindwa kufahamu kwamba fedha ya taifa ni kitu kinachoonesha uwezo na uhuru wa kiuchumi. Fedha ya nchi yetu inajulikana kama shilingi ya Tanzania ambayo imetengenezwa kwa mfumo wa noti na sarafu, na haina rangi nne za kijani, bluu, nyeusi na njano.

Zaidi, baadhi ya wanafunzi waliooanisha na kipotoshi C, *Mwenge wa Uhuru,* walishindwa kubaini kuwa Mwenge wa Uhuru huonesha uhuru na nuru ya taifa letu la Tanzania, tofauti na bendera ya taifa ambayo huonesha uhuru, asili ya watu na rasilimali za taifa.

Aidha, wanafunzi waliooanisha na kipotoshi D, *Mnyama wa Taifa* ambaye ni twiga, walishindwa kutofautisha dhana ya Mnyama wa Taifa na alama ya taifa inayowakilisha uhuru wa taifa letu, ambayo ni Bendera ya Taifa. Wanafunzi hawa walishindwa kutambua kwamba Mnyama wa Taifa (twiga) ni alama inayoonesha uwepo wa utajiri na urithi wa maliasili na kwamba mnyama twiga ni kivutio cha utalii nchini Tanzania.

Aidha, baadhi ya wanafunzi waliooanisha na kipotoshi E, *Nembo ya Taifa,* wanafunzi hawa hawakuwa na uelewa wa kutosha, kwamba nembo ya taifa ni alama inayoonesha umiliki wa nyaraka za serikali kama vile katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nembo ya taifa, na kwamba ina jumla ya vipengele 13 (kumi na tatu) vyenye kuwasilisha maudhui tofauti ya nchi.

Mwisho, wanafunzi wengine walioanisha na kipotoshi F, *Wimbo wa Taifa* walishindwa kuelewa kwamba Wimbo wa Taifa ni wimbo

rasmi unaoimbwa kwenye matukio muhimu; kwa mfano, Rais anapotaka kulihutubia taifa au kipindi anapozuru taifa jingine, au wakati wa michezo ya kimataifa inapohusisha nchi yetu. Wimbo wa taifa pia ni sala kwa Tanzania na Waafrika wote.

Katika Kipengele (iii), swali lilimtaka mwanafunzi kuoanisha alama ya taifa kutoka Orodha B inayoendana na maelezo ya Orodha A, ambayo ni alama inayoonesha picha ya mwanaume upande wa kushoto na mwanamke upande wa kulia. Wanafunzi waliokuwa na uelewa wa kutosha walichagua jibu sahihi E, *Nembo ya Taifa*. Wanafunzi hawa walijua kuwa nembo ya taifa la Tanzania ni alama inayoakisi urithi, historia na matarajio ya nchi. Ina vipengele kadhaa vinavyobeba maana tofauti, kama vile; ngao na mikuki, sura ya mwanamume na mwanamke, na kauli mbiu. Nembo ya taifa ina faida kadhaa kama vile; ishara ya umoja na utambulisho wa taifa, kuakisi historia ya taifa na mapambano, uwakilishi wa kitamaduni, mwamko wa mazingira, msukumo wa maendeleo na ukuaji, kuimarisha mamlaka ya kitaifa na kutambuliwa kimataifa.

Wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *Bendera ya Taifa,* hawakuwa na uelewa sahihi wa alama za taifa. Hawakuelewa kuwa bendera ya taifa hupepea katika maeneo maalum, kama vile ofisi za serikali na taasisi mbalimbali, kama vile shule. Bendera ya taifa hupandishwa saa 12 asubuhi na kushushwa saa 12 jioni. Alama hii ya taifa ikiwa inapandishwa au kushushwa kila mmoja anapaswa kusimama kwa ukakamavu kama ishara ya kuliheshimu taifa.

Vilevile, baadhi ya wanafunzi waliochagua kipotoshi B, *Fedha ya Taifa* hawakujua kuwa fedha ya taifa letu inaitwa shilingi na ipo katika mfumo wa sarafu na noti. Wanafunzi hawa walitakiwa kutambua kuwa alama hii ya taifa hutumika pia kununulia bidhaa na kulipia huduma mbalimbali.

Hata hivyo, wanafunzi wengine walioanisha na kipotoshi C, *Mwenge wa Uhuru*, walishindwa kuelewa kuwa Mwenge wa Uhuru humulika nchi yetu pamoja na mipaka, huleta tumaini, upendo na heshima kwa watanzania juu ya wajibu wao wa kuilinda na kuitetea nchi yao.

Wanafunzi wengine walichagua kipotoshi D, *Mnyama wa Taifa.* Alama hii inaonesha uwepo wa utajiri na urithi wa maliasili ya taifa. Twiga ni kivutio cha utalii nchini Tanzania. Aliyechagua kipotoshi D*, mnyama wa taifa,* alishindwa kutofautisha dhana ya mnyama wa taifa na alama inayowakilisha nembo ya taifa. Aidha, alikosa maarifa sahihi ya kutofautisha nembo ya taifa na twiga ambaye ni kielelezo na alama ya Taifa.

Aidha, baadhi ya wanafunzi waliooanisha na kipotoshi E, *Nembo ya Taifa*, hawakujua kuwa Nembo ya Taifa ni kielelezo cha uhuru na nguvu ya taifa katika kujihami na kujilinda. Nembo ya Taifa ina sehemu kuu Nne: sehemu ya dhahabu inayojumuisha mwenge wa uhuru, bendera ya taifa yenye rangi Nne, sehemu yenye rangi nyekundu inayomaanisha ardhi yenye rutuba, sehemu yenye milia bluu na nyeupe inayomaanisha mawimbi ya bahari na maziwa.

Mwisho, wanafunzi waliochagua kipotoshi F, *Wimbo wa Taifa,* hawakuwa na uelewa kuwa wimbo huu huimbwa katika matukio muhimu ya kitaifa kama vile Rais, makamu wa Rais na Waziri Mkuu wanapozuru nchi nyingine. Kwa kuongezea, huimbwa pia wakati Rais wa nchi nyingine anapozuru nchi yetu, kabla na baada ya Rais kulihutubia taifa. Pia, wimbo wa Taifa huimbwa kipindi kiongozi wa ngazi ya juu anapofariki. Vilevile, wanafunzi hawa hawakutambua kuwa wimbo wa taifa huimbwa shuleni na wakati timu za taifa zinapocheza na timu za mataifa mengine.

Kipengele (iv) kiliwataka wanafunzi kuoanisha alama ya taifa kutoka Orodha B inayoendana na alama inayoonesha uzalendo kwa taifa letu kutoka Orodha A. Wanafunzi waliokuwa na uelewa wa kutosha walichagua jibu sahihi F, *Wimbo wa Taifa*. Wanafunzi hawa walielewa kuwa wimbo wa taifa ni alama ya taifa ambayo huimbwa katika matukio muhimu ya kitaifa. Wimbo wa Taifa una maneno yanayoonesha maombi kwa Mungu aibariki Tanzania, afanikishe umoja, amani na mshikamano. Pia, ni ishara ya umoja wa taifa, huchochea uzalendo na mapenzi ya nchi, hutumika kuwakilisha nchi kwenye michezo ya kimataifa na huweka hisia za heshima na utambulisho wa taifa.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *Bendera ya Taifa*, walishindwa kutambua kuwa Bendera ya Taifa ni kipande cha kitambaa kinachowakilisha uhuru wa nchi. Bendera ya taifa ina jumla ya rangi Nne ambazo ni kijani, manjano, nyeusi na bluu. Wanafunzi hawa hawakuelewa kwamba bendera ya taifa inapepea maeneo mbalimbali, kama vile shuleni, vituo vya afya na ofisi mbalimbali za umma.

Wanafunzi wengine walichagua kipotoshi B, *Fedha ya Taifa.* Wanafunzi hawa hawakutambua kwamba fedha ya taifa haitumiki kuwakilisha uzalendo katika nchi yetu, bali inatumika kwa manunuzi ya bidhaa na malipo ya huduma mbalimbali. Fedha ya Tanzania inaitwa shilingi, na ipo katika mfumo wa sarafu na noti.


Baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi C, *Mwenge wa Uhuru.* Wanafunzi hawa hawakuwa na uelewa kuwa Mwenge wa Uhuru ni alama ya taifa inayomulika nchi na mipaka yake, huleta matumaini, upendo na heshima kwa watanzania wote tofauti na Bendera ya Taifa ambayo inaoonesha uhuru kamili wa taifa, asili ya watu na rasilimali za taifa. Zaidi ya hapo, baadhi ya wanafunzi walichagua Kipotoshi D, *Mnyama wa Taifa*. Wanafunzi hawa walishindwa kutambua kuwa mnyama wa taifa ni twiga. Picha ya twiga hutumika kama alama ya usalama kwenye pesa ya noti ya Tanzania.

Mwisho, kuna wanafunzi waliochagua kipotoshi E, *Nembo ya Taifa*. Wanafunzi hawa hawakutambua kuwa Nembo ya Taifa ni kielelezo cha umoja, uhuru na nguvu ya taifa. Walitakiwa kutambua kuwa wakati mwingine nembo hii hutumika kama muhuri wa taifa katika ofisi za serikali.

## 2.3 Swali la 3: Kuwa Mstahimilivu

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa Mstahimilivu*. Liliwataka wanafunzi kujibu kipengele cha (i) – (iv) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri, kwani wanafunzi 1,143,423 (74.71%) walifaulu kwa kupata alama 4

hadi 8. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa wanafunzi waliopata alama 8 walikuwa 400,428 (26.16%). Vilevile, wanafunzi 435,428 (28.45%) walipata alama 6 na wanafunzi 307,567 (20.10%) walipata alama 4. Aidha, wanafunzi 387,059 (25.29%) walipata alama 0 hadi 2, hivyo hawakufaulu. Chati Na. 3 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 3.




**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 3*

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele

(i) Hamis ana ratiba ya kila siku na anajua anataka kuwa nani. Hivyo, Hamis anaonekana kuwa na

________________________________________

(malengo, ufanisi, maadili)

Kipengele hiki cha swali kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kufikia malengo aliyojiwekea kwa kuwa na mtazamo chanya.* Kilipima uelewa wa mwanafunzi kuhusu umuhimu wa kuwa na ratiba ya kila siku katika kutimiza majukumu ili kufikia malengo yake, na kuwa na mtazamo chanya. Jibu sahihi lilikuwa ni *malengo.* Jibu hili lilibainishwa na wanafunzi walioelewa kuwa malengo ni matarajio au vitu ambavyo mtu au kikundi kinakusudia kufanikisha katika kipindi fulani. Faida zake ni pamoja na kuwa na mwelekeo, motisha, kupima mafanikio na matumizi bora ya muda na rasilimali.

Wanafunzi hawa walikuwa na uelewa kwamba ratiba ya kila siku humsaidia mtu kufikia malengo aliyojiwekea. Hivyo, ili kufikia malengo katika maisha mtu anapaswa kuwa na ratiba na kuitekeleza ipasavyo. Kwa mfano, ili mwanafunzi aweze kufikia malengo yake ya kufanya vizuri kitaaluma anapaswa kuwa na ratiba yake binafsi ya kujisomea na kuifuata ipasavyo.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua jibu lisilo sahihi *ufanisi* walipaswa kuelewa kuwa ufanisi ni kutenda jambo kwa kutumia ujuzi na maarifa ili kuwa na matokeo ya kiwango cha juu kilichokusudiwa. Aidha, ufanisi ni uwezo wa kutumia rasilimali kwa njia iliyobora ili kufanikisha malengo kwa muda mfupi. Ufanisi huokoa rasilimali, huboresha ubora wa kazi. Wanafunzi hawa walishindwa kutambua kuwa ratiba ni msaada mkubwa kwa mtu anayetaka kufanya kazi yake kwa ufanisi ili aweze kufikia malengo yake. Kwa mfano, mwanafunzi anapoandaa ratiba yake na kuitekeleza ipasavyo inamfanya kuwa na ufanisi mkubwa katika taaluma.

Vivyo hivyo, wanafunzi wengine walichagua kipotoshi *maadili.* Wanafunzi hawa hawakutambua kuwa maadili ni matendo au tabia zinazokubalika katika jamii, kanuni au misingi inayotawala tabia ya mtu au jamii kuhusu mema na mabaya, haki na dhuluma. Maadili yanajenga uaminifu, yanaimarisha mahusiano, yanakuza nidhamu, na yanasaidia maendeleo endelevu. matendo hayo ni kama nidhamu, uadilifu, upendo, utii, uzalendo, ukarimu na kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na jamii au nchi. Hata hivyo, maadili ni mafundisho yanayotolewa katika nafasi mbalimbali, hasa katika malezi ili kuelekeza binadamu atende kwa namna ambayo itamjenga yeye na jamii nzima. Wanafunzi hawa walitakiwa kuelewa kwamba ili mtu aweze kufikia malengo yake na kufanikiwa kimaisha, anatakiwa kuwa na maadili mema yanayokubalika katika jamii.

(ii) Kwa nini tunajifunza kutokana na makosa ya watu wengine?

__________________________________________

(ili kuwacheka, ili kuwafuata, ili kuyaepuka.)

Kipengele hiki cha swali kilitoka katika umahiri mahususi wa *kujifunza kwa kuchanganua mambo kiyakinifu.* Kilipima uelewa wa wanafunzi kuhusu kujifunza kutokana na makosa ya watu wengine, na kuyatendea kazi. Wanafunzi waliokuwa na uelewa wa kutosha walichagua jibu sahihi *ili kuyaepuka.* Wanafunzi hawa walielwa kuwa, katika maisha ya kila siku, watu hufanya makosa mbalimbali ambayo mtu au watu wanapaswa kuyatumia kama zana ya kufundishia ili wasiyarudie tena siku zijazo. Wanafunzi hawa walikuwa na uelewa kwamba katika jamii hatupaswi kujifunza mambo mazuri tu, bali hata mabaya tunayopaswa kuchukua kama somo ili tusiyarudie katika maisha yetu ya kila siku. Kujifunza kutokana na makosa hupunguza maumivu na madhara, huokoa wakati na rasilimali, huboresha maamuzi yetu, husaidia kupata mtazamo mzuri na huongeza hekima na ufahamu.

Vivyo hivyo, waliochagua *ili kuwacheka* walipaswa kuelewa kwamba kuwacheka watu ni kinyume cha maadili na endapo watafanya hivyo, watapoteza malengo yao. Kumcheka mtu aliyekosea hakusaidii bali kutamfanya akose kujiamini na kufanya makosa zaidi. Mtu aliyekosea anahitaji upendo, ushauri na kutiwa moyo ili aweze kutenda vyema kama wengine. Wanafunzi hawa walipaswa kuelewa kuwa kumcheka mtu anapokosea kunaweza kusababisha chuki na ugomvi katika jamii. Madhara mengine ya kumcheka mtu aliyekosea ni kumvunja moyo, kumletea unyonge wa kihisia, kuwafanya watu wengine kuogopa kujifunza, kuongeza msongo wa mawazo na kukosa msaada wa kujirekebisha. Badala ya kucheka makosa ya wengine ni vyema kuwaonea huruma na kuwasaidia kujifunza kwa kutumia lugha ya upole na kuwaonesha njia bora.

Wanafunzi waliochagua jibu lisilo sahihi *ili kuwafuata,* ni dhihiri hawakujua kwamba kufuata makosa ya wengine kutawapotezea mwelekeo na malengo katika maisha. Wanafunzi hawa walitakiwa kuelewa kwamba kufuata makosa ya wengine kunaweza kumpoteza mtu kwa kujiingiza kwenye mambo yasiofaa katika jamii, kama vile ulevi na unywaji pombe wa kupindukia, unaosababisha magonjwa ya figo, ini na kisukari. Pia,

kutamsababishia mtu kupoteza maadili, kuchanganyikiwa, kushindwa kujitambua, kutengwa na jamii, na kuingia matatizoni; kutumia madawa ya kulevya; wizi; kupata magonjwa kama vile UKIMWI, kifua kikuu; na kushiriki ngono kwenye umri mdogo, kunakosababisha kuacha shule, mimba za utotoni, na kupoteza muelekeo wa maisha. Hivyo, katika jamii tunapaswa kuwafuata wale watu wanaotenda matendo mazuri na yanayokubalika katika jamii zetu. Ni muhimu kujiepusha na mazingira au watu wanaoweza kumvuta mtu katika tabia au matendo yasiyofaa.

(iii) Matumizi ya madawa ya kulevya yana madhara gani kwa mtumiaji?

____________________________________________

(Huharibu malengo yake, Huharibu ubunifu wake, Huharibu furaha yake)

Kipengele hiki cha swali kilitoka katika umahiri mahususi wa *kujifunza kwa kuchanganua mambo kiyakinifu*. Kilipima uelewa wa wanafunzi kuhusu madhara ya matumizi ya madawa ya kulevya. Katika swali hili, wanafunzi waliokuwa na uelewa wa kutosha walichagua jibu sahihi *Huharibu malengo yake.* Wanafunzi hawa walielewa kuwa malengo ni mipango ambayo mtu ameweka kwa ajili ya kutimiza, au kufikia kitu fulani katika muda fulani. Wanafunzi hawa walitambua kuwa katika maisha yetu ya kila siku kuna vitu vinavyochangia katika kuharibu malengo ya watu. Kwa mfano, uvivu, utoro shuleni na kutowasikiliza walimu na wazazi. Kwa upande mwingine, matumizi ya madawa ya kulevya kama bangi, mirungi na matumizi ya mihadarati yanasababisha mtumiaji kuwa na uraibu unaomfanya kushindwa kabisa kufanya kazi ili kujipatia kipato cha kila siku, na pia kusababisha madhara makubwa kiafya, hivyo mtu kushindwa kabisa kufikia malengo yake. Madhara mengine ya madawa ya kulevya ni uharibifu wa viungo kama ini, figo na mapafu. Vilevile, huweza kumweka mtu katika hatari ya kupata magonjwa kama VVU/UKIMWI, na utegemezi wa madawa ya kulevya, magonjwa ya akili, migogoro ya kifamilia, uhalifu, kutengwa na jamii, na umasikini. Kwa ujumla, matumizi ya madawa

ya kulevya yana madhara makubwa yanayoathiri afya, mahusiano, na maisha ya mtumiaji.

Wanafunzi wengine waliandika jibu lisilo sahihi, *Huharibu furaha yake.* Wanafunzi hao hawakujua kuwa madawa ya kulevya hurejelea matumizi mabaya au hatari ya vitu vinavyoathiri akili. Mara nyingi huhusisha kutumia madawa kwa njia ambayo huathiri vibaya afya ya mtu, ustawi wa akili, na utendaji wa kila siku. Wanafunzi hawakujua kuwa utumiaji wa dawa za kulevya huleta furaha kwa muda mfupi, na baada ya hapo humsababishia mtumiaji kuwa na uraibu unaomfanya ajisikie vibaya na kuwa kama mgonjwa. Matumizi mabaya ya dawa za kulevya yana madhara makubwa kwa karibu kila nyanja ya maisha ya mtumiaji, yanayoathiri afya zao, mahusiano ,na ubora wa maisha kwa ujumla. Kwa ujumla matumizi ya dawa hayawezi kuleta furaha kwa mtumiaji, bali yanageuka kuwa changamoto kubwa inayohitaji matibabu na ushauri.

Vile vile, wanafunzi waliochagua *Huharibu ubunifu wa mtu* hawakujua kuwa ubunifu ni mchakato wa kutumia fikra za kimantiki au tajriba kuunda suluhu la kipekee kwa changamoto, kutambua vitu kama vile teknolojia au ujuzi mpya. Wanafunzi hawa walitakiwa kuelewa kuwa matumizi ya dawa husababisha mtumiaji kutofikia malengo, kwa sababu humpunguzia mtumiaji uwezo wa kufikiri na kuwa na ufanisi mdogo katika utendaji wa kazi.

(iv) Unaposhindwa kutatua changamoto unashauriwa kufanya nini?

_______________________________________________

(kulalamika, kukimbia, kuomba ushauri)

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi wa *kuwa mvumilivu katika maisha ya kila siku*. Swali lilipima uelewa wa wanafunzi kuhusu hatua za kuchukua mtu anaposhindwa kutatua changamoto. Wanafunzi wenye uelewa wa kutosha walichagua jibu sahihi, ambalo ni *Kuomba ushauri.* Wanafunzi hawa walitambua kuwa ushauri ni mchakato wa kutoa au kupokea maoni, mawazo au

mapendekezo kuhusu jambo fulani kwa lengo la kumsaidia mtu kufanya uamuzi bora. Changamoto ni hali yoyote inayotokea, ambayo inakwamisha au kuzuia mtu, kikundi au jamii kufanikisha malengo yao. Changamoto hupunguza maendeleo, hufifisha ndoto za mtu, na kuchochea migogoro. Changamoto katika maisha ni jambo lisiloepukika, na endapo hazitatatuliwa ipasavyo huweza kuathiri ustawi wa mtu. Wanafunzi hawa walielewa kuwa njia pekee ya kutatua changamoto katika maisha ni kuomba ushauri kwa watu sahihi; kwa mfano, walimu au wazazi. Ushauri una faida nyingi kama vile kutoa mwongozo, kusaidia kufanya maamuzi bora, kuongeza uelewa, kupunguza makosa, kuimalisha mahusiano, kujenga kujiamini na kusaidia kufanikisha malengo. Njia nyingine za kutatua changamoto ni kuelewa chanzo, kubainisha malengo, kushirikiana na wengine, kusikiliza na kujifunza kutoka kwa wengine. Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi swali la 3.

3. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.

(i) Hamis ana ratiba ya kila siku na anajua anataka kuwa nani. Hivyo, Hamis anaonekana kuwa na malengo.

(malengo, ufanisi, maadili)

(ii) Kwa nini tunajifunza kutokana na makosa ya wengine?

ili kuyaepeka.

(ili kuwacheka, ili kuwafuata, ili kuyaepuka)

(iii) Matumizi ya madawa ya kulevya yana madhara gani kwa mtumiaji?

Huharibu malengo yake.

(Huharibu malengo yake, Huharibu ubunifu wake, Huharibu furaha yake)

(iv) Unaposhindwa kutatua changamoto unashauriwa kufanya nini?

kuomba ushauri.

(kulalamika, kukimbia, kuomba ushauri)

**Kielelezo Na. 1.1:** *Sampuli ya Majibu Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 3*

Hata hivyo, wanafunzi waliochagua jibu lisilo sahihi *Kulalamika,* hawakuelewa kuwa kulalamika ni kueleza huzuni, maumivu, kutoridhika au kutafuta kosa kwa jambo mtu alilotendewa. Kulalamika kunaleta kunyong'onyea, kuwa na ugomvi, kugombana na watu, na kuleta taharuki. Kwa hiyo, mtu anaposhindwa kutatua matatizo na kuanza kulalamika hakumsaidii bali kunamuongezea changamoto. Hivyo, njia nzuri ya kutatua changamoto ni kuomba ushauri kwa watu sahihi.

Aidha, wanafunzi waliochagua jibu lisilo sahihi *kukimbia* hawakujua kuwa kukimbia changamoto ni kutokutaka utatuzi wa tatizo linalomkumba mtu na kuamua kuliacha. Kukimbia changamoto hakumsaidii mtu badala yake kunamuongezea matatizo. Mtu anapopata changamoto, anatakiwa kukaa chini na kutafakari kuhusu makossa aliyoyafanya na kutafuta njia za kutatua changamoto hizo ili alete mafanikio zaidi katika maisha yake. Wanafunzi hawa hawakuelewa kwamba changamoto ni sehemu ya maisha ya mwanadamu na ni jambo lisiloepukika. Ikiwa changamoto hizo hazitatatuliwa ipasavyo, zinaweza kumzuia mtu kufikia malengo aliyokusudia.

Hasara za kukimbia changamoto ni nyingi, ikiwa ni pamoja na kupoteza fursa, kukosa kujifunza, kudhoofisha ujasiri, kuongeza msongo wa mawazo. na kukosa mafanikio. Mtu anaposhindwa kutatua changamoto zinazomkabili, anashauriwa kutulia na kuomba ushauri kwa watu anaowaamini wanaweza kumsaidia, badala ya kulalamika au kukimbia changamoto hizo. Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi ambaye aliandika majibu yasiyo sahihi katika swali la 3.

3. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.

(i) Hamis ana ratiba ya kila siku na anajua anataka kuwa nani. Hivyo, Hamis anaonekana kuwa na ___tabia njema___

(malengo, ufanisi, maadili)

(ii) Kwa nini tunajifunza kutokana na makosa ya wengine?

___malengo ufanisi maadili___

(ili kuwacheka, ili kuwafuata, ili kuyaepuka)

(iii) Matumizi ya madawa ya kulevya yana madhara gani kwa mtumiaji?

___Kunywa madawa ya kulevya___

(Huharibu malengo yake, Huharibu ubunifu wake, Huharibu furaha yake)

(iv) Unaposhindwa kutatua changamoto unashauriwa kufanya nini?

___Kutatua changamoto___


(kulalamika, kukimbia, kuomba ushauri)

**Kielelezo Na. 1.2:** *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyo sahihi katika Swali la 3*

## 2.4 Swali la 4: Kuheshimu Jamii

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuheshimu jamii*. Swali lilikuwa na vipengele vinne (i) - (iv) ambavyo vilimtaka mwanafunzi kukamilisha aya kwa kuandika maneno yanayokosekana katika nafasi zilizotolewa.

Ufaulu katika swali hili ulikuwa ni wa wastani, kwa kuwa wanafunzi 997,332 (65.16%) walipata alama 4 hadi 8. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa wanafunzi waliopata alama 8 walikuwa 260,872 (17.04%), na wanafunzi 335,679 (21.93%) walipata alama 6. Aidha, wanafunzi 400,781 (26.19%) walipata alama 4. Pia, wanafunzi 533,180 (34.84%) walipata alama 0 hadi 2, hivyo hawakufaulu. Chati Na. 4 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4*

Uchambuzi wa swali ulikuwa kama ifuatavyo:


Kamilisha aya ifuatayo kwa kwa kuandika maneno yanayokosekana katika nafasi zilizotolewa katika vipengele (i) - (iv).

*Jina la Tanzania limetokana na muungano wa nchi mbili ambazo ni (i) _________________ na (ii) __________________Nchi hizo ziliungana na kuunda nchi ya Tanzania mwaka_____________(iii) _________________. Wakati huo viongozi wa nchi hizo walikuwa Julius K. Nyerere na (iv) _____________________.*

Kipengele (i) na (ii) vilimtaka mwanafunzi kuandika nchi mbili zilizoungana kuunda nchi ya Tanzania. Wanafunzi waliokuwa na maarifa ya kutosha waliandika majibu sahihi ambayo ni *Tanganyika na Zanzibar.* Wanafunzi hawa walijua kuwa asili ya Tanzania ya kijiografia, kihistoria na kiutamaduni ni nchi iliyozaliwa kutokana na muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Tanganyika ilipata uhuru wake tarehe 9, Desemba 1961 na Zanzibar ni visiwa vilivyopo katika bahari ya Hindi, na ilipata uhuru wake tarehe 10, Desemba 1963. Mara tu baada ya mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12, Januari 1964, Tanganyika na Zanzibar ziliungana tarehe 26/04/1964 na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi waliandika majibu yasiyo sahihi, kama vile *Tanzania na Zanzibar*. Wanafunzi hawa hawakuwa na uelewa kuwa kabla ya mwaka 1964 hakukuwa na nchi iliyokuwa inaitwa Tanzania, bali nchi hiyo ilitwa Tanganyika. Wengine waliandika *Zanzibar na Kenya.* Wanafunzi hawa hawakuwa na uelewa kuwa Kenya ni nchi jirani inayopakana na Tanzania upande wa Kaskazini Mashariki, na ni nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wanafunzi wengine waliandika mwaka 1977, hivyo hawakujua kuwa ni mwaka ambao chama cha TANU kiliungana na chama cha AFROSHIRAZ, kisha kuunda Chama Cha Mapinduzi (CCM). Aidha, wengine waliandika mwaka 1995, na hii inaashiria kwamba wanafunzi hao hawakuelewa kwamba mwaka huu ndipo kulifanyika uchaguzi wa kwanza uliohusisha vyama vingi nchini. Wanafunzi wengine waliandika majina ya makabila yanayopatikana Tanzania, kama vile *Wasambaa na Wamasai.*

Kipengele (iii) kilimtaka mwanafunzi kuandika mwaka ambao nchi hizo mbili ziliungana kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wanafunzi waliokuwa na maarifa ya kutosha waliandika jibu sahihi ambalo ni mwaka *1964.* Wanafunzi hao walielewa kuwa mnamo tarehe 26/04/1964 Marais wa kwanza wa Tanganyika na Zanzibar walichanganya udongo wa nchi hizo kuashiria muungano. Baada ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar mnamo mwaka 1964, matukio muhimu kadhaa yalitokea ambayo yalichangia katika muktadha wa kisiasa, kijamii na kiuchumi. Baadhi ya matukio hayo ni kuundwa kwa serikali ya muungano, mabadiliko ya kisiasa, *Afro-Shirazi Party (*ASP) kiliungana na TANU na kuunda chama kipya cha mapinduzi (CCM) mwaka 1977, kuundwa kwa katiba na utekelezaji wa Sera ya Ujamaa na kujitegemea. Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 4.


4. Kamilisha aya ifuatayo kwa kuandika maneno yanayokosekana katika kipengele (i) – (iv).

Jina la Tanzania limetokana na muungano wa nchi mbili ambazo ni (i) Tanganyika na (ii) Zanzibar. Nchi hizo ziliungana na kuunda nchi ya Tanzania mwaka (iii) 1964. Wakati huo viongozi wa nchi hizo walikuwa Julius K. Nyerere na (iv) Sheikh Abedi Amani Karume.


**Kielelezo Na. 2.1:** *Sampuli ya Majibu Sahihi ya Mwanafunzi Katika Swali la 4*

Baadhi ya wanafunzi waliandika majibu yasiyo sahihi, kama vile *1961*. Wanafunzi hawa hawakuelewa kuwa mwaka 1961 ni mwaka ambao nchi ya Tanganyika ilipata uhuru wake kutoka kwa nchi ya Uingereza, na ni mwaka ambao Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitangazwa kuwa Waziri Mkuu wa kwanza wa Tanganyika. Wanafunzi wengine waliandika mwaka *1999,* ikiashiria wanafunzi hawa kutoelewa kwamba mwaka huu ndio mwaka ambao Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alifariki. 1977 ambao ni mwaka wa kuzaliwa kwa Chama cha Mapinduzi (CCM), kufuatia kuungana kwa vyama vya *Afro-Shiraz party* (ASP na TANU). Pia ni mwaka ambao katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 iliandikwa.

Kipengele (iv) kilimtaka mwanafunzi kuandika majina ya muasisi wa muungano wa Tanganyika na Zanzibar aliyeshirikiana na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Wanafunzi waliokuwa na uelewa wa kutosha waliandika jibu sahihi *Sheikh Abeid Amani Karume.* Wanafunzi hawa walitambua kuwa Abeid Amani Karume aliyekuwa Rais wa kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar alishirikiana kwa ukaribu na Mwalimu Julius K Nyerere kukamilisha muungano wa Tanganyika na Zanzibar mnamo mwaka 1964. Viongozi hao wawili walichanganya udongo wa nchi mbili kama

ishara ya muungano. Mchango wake katika muungano ni pamoja na kutoa ushirikiano wa kisiasa kwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, hasa katika kuimarisha mshikamano wa kisiasa, kiuchumi na kijamii, kutia saini hati ya muungano tarehe 22/04/1964, kukubali kujenga nchi ya pamoja, kuimarisha utulivu wa kisiasa na kudumisha umoja wa Afrika.

Kwa upande wa mwingine, baadhi ya wanafunzi waliandika majibu yasiyo sahihi kwa kutaja majina ya viongozi waliopita kama vile *Jakaya Mrisho Kikwete.* Wanafunzi hawa walishindwa kutambua kwamba Jakaya Mrisho Kikwete alikuwa Rais wa awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka mwaka 2005 hadi mwaka 2015. Wanafunzi wengine waliandika jina la aliyewahi kuwa Rais wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *Hayati Ali Hassan Mwinyi,* aliyekuwa Rais wa Tanzania kuanzia mwaka 1985 hadi 1995*.* Wanafunzi wengine waliandika jina la Rais wa sasa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *Samia Suluhu Hassan*. Wanafunzi hawa hawakuwa na uelewa kuwa Samia Suluhu ni Rais wa kwanza mwanamke nchini Tanzania, na kwamba alliingia madarakani baada ya kifo cha Hayati Daktari John Pombe Magufuli aliyekuwa Rais wa awamu ya tano. Kwa kumalizia, wanafunzi wengine waliandika majina ya watu waliokuwa viongozi katika ngazi mbalimbali kama vile Rashid Mfaume Kawawa aliyekuwa Waziri Mkuu wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; wengine waliandika jina la kiongozi *Kenneth* Kaunda Rais wa kwanza wa nchi ya Zambia. Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyo sahihi katika swali la 4.



4. Kamilisha aya ifuatayo kwa kuandika maneno yanayokosekana katika kipengele (i) – (iv).


Jina la Tanzania limetokana na muungano wa nchi mbili ambazo ni (i) Tanganyika na (ii) Unguja. Nchi hizo ziliungana na kuunda nchi ya Tanzania mwaka (iii) 1977. Wakati huo viongozi wa nchi hizo walikuwa Julius K. Nyerere na (iv) Ali Hasani Mwinyi

**Kielelezo Na. 2.2:** *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika Swali la 4*

## 2.5 Swali la 5: Kuwa Mwajibikaji


Swali hili lilitoka katika umahiri Mkuu wa *Kuwa Mwajibikaji* na Umahiri Mahususi wa *kusimamia majukumu yanayomhusu nyumbani na shuleni*. Swali lilipima uwezo wa wanafunzi kutambua wajibu wao katika ngazi ya familia. Walipewa picha ili kuichunguza kwa makini, kisha kujibu maswali katika vipengele (a) - (b).

Ufaulu katika swali hili ulikuwa ni wa kiwango kizuri ikilinganishwa na maswali mengine, kwani wanafunzi 1,283,591 (83.86%) waliofanya swali hili walifaulu kwa kupata alama 4 hadi 8. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa wanafunzi waliopata alama 8 walikuwa 734,409 (47.98%). Vilevile, wanafunzi 415,991 (27.18%) walipata alama 6, na wanafunzi 133,191 (8.70%) walipata alama 4. Uchambuzi zaidi wa takwimu unaonesha kuwa wanafunzi 246,921 (16.14%) walipata alama 0 hadi 2, hivyo hawakufaulu. Chati Na. 5 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 5.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 5*

Ufuatao ni uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 5.



## Maswali:

(a) Taja jina la wanyama waliopo kwenye picha ____________

Swali hili lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kubaini jina la wanyama wanaoonekana katika picha. Wanafunzi wenye umakini na uelewa walibaini kwa usahihi kuwa wanyama wanaooneka katika picha ni *Ng'ombe*. Wanafunzi hawa walijua kuwa ng'ombe ni mnyama mkubwa mwenye mwili mwepesi na manyoya mafupi au marefu, kutegemea na aina yake, ana miguu minne, anayefugwa na binadamu na anakula majani. Wanafunzi hawa walikuwa nauelewa kuwa ng'ombe hufungwa kwa ajili ya nyama, maziwa, mbolea, pato la fedha, bidhaa za ngozi, wanyama kazi (kulima/kubeba mizigo) na usalama wa chakula. Wanafunzi hawa walijua kuwa kuna ufugaji wa ng'ombe wa aina mbili, ambazo ni ufugaji wa ndani na nje.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwepo kwa wanafunzi waliotaja majibu yasiyo sahihi, kama vile *Twiga, Simba, Zizini* na *Mbuzi.* Wanafunzi hawa walionekana kukosa maarifa juu ya wanyama wafugwao kama ng'ombe. Pia, wanafunzi hawa hawakujua kuwa twiga ni mnyama mrefu na ndiye mnyama pekee mwenye shingo ndefu. Ana mwili mrefu na miguu mirefu, ngozi yake ina michoro ya rangi ya shaba, nyeupe au njano. Anakula majani ya miti na mimea ya majani ya juu. Anaweza kufikia urefu wa mita 5 hadi 6.5. kwa sifa hizo, wanyama wanaoonekana katika picha siyo Twiga. wanafunzi hawa walitakiwa kuelewa kwamba mnyama Twiga hawawezi kufugwa na binadamu, kwani ni wanyama wasiofugwa na makazi yao ni kwenye mbuga za wanyama na hifadhi za Taifa.

Wanafunzi walioandika *Simba,* hawakujuwa kuwa ni mnyama mkubwa mwenye mwili mzito na ndevu (dume), wana rangi ya njano au rangi ya shaba. Ni mnyama anayekula nyama, na huishi katika maikundi. Hivyo, wanyama wanaoonekana katika picha hawawezi kuwa simba.

Vivyo hivyo, walioandika *Mbuzi*, hawakuelewa kuwa mbuzi ni mnyama wa ukubwa wa kati na ana manyoya ya rangi mbalimbali kutoka nyeupe, kahawia hadi nyeusi; wana pembe za kurudi nyuma na wanapenda kula majani na mimea ya aina nyingi. Kwa sifa hizo, wanyama wanaoonekana katika picha hawawezi kuwa mbuzi, hasa ukizingatia kimo chao.

Wanafunzi walioandika *Zizini,* walitakiwa kufahamu kuwa zizi ni sehemu au uwanja wa kufugia wanyama hasa ng'ombe, kondoo, au mbuzi. Inakuwa ni sehemu maalumu iliyotengwa na uzio au kuta kwa ajili ya wanyama hao ili wasiende mbali. Zizini pia siyo jibu sahihi kulingana na kinachoonekana katika picha.

(b) Mtu anayeonekana katika picha anafanya nini? __________

Swali hili lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kutambua kitendo anachofanya mtu katika picha. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa majibu sahihi yalikuwa *analisha ng'ombe* au *anawapa ng'ombe chakula.* Wanafunzi waliojibu kwa usahihi walijua kuwa ng'ombe wakiwa zizini, wanalishwa majani mabichi au makavu kwa msimu wa kiangazi, lakini pia wanapewa vyakula vya ziada kama "*silage"* pamoja na maji.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi walioandika majibu yasiyo sahihi hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu wajibu na majukumu ya mtoto awapo nyumbani. Baadhi ya majibu yasiyo sahihi yaliyoandikwa na wanafunzi yalikuwa kama ifuatavyo: *anawafunga Ng'ombe,* wanafunzi hawa hawakujua kuwa kufunga ng'ombe ni kitendo cha kumfungia ng'ombe katika sehemu maalumu kama banda au zizi kwa ajili ya kulinda, kumlisha au kumtunza kwa usalama.

Wanafunzi walioandika *kumfungulia ng'ombe* hawakujua kuwa ni kumwachia ng'ombe kutoka kwenye zizi au banda ili aweze kutoka na kula majani, au kufanya shughuli nyingine. Wanafunzi wengine walioandika *kukamua maziwa*, hawakujua kuwa ni mchakato wa kuvuta maziwa kwa tezi za ng'ombe. Hata hivyo, walishindwa kubaini kuwa mtu anayemkamua ng'ombe maziwa hukaa ubavuni

mwa ngo’mbe ndani ya zizi, akiwa na vifaa vya kukamulia kama vile jagi na kikombe. Baadhi ya wanafunzi waliandika jibu lisilo sahihi *batii;* hawa walikosa uelewa kuwa bati ni aina ya chuma kinachotumika kufunika paa la nyumba.

Aidha, wengine walishindwa kuhusianisha vitu vilivyopo ndani ya picha hiyo, kama vile *toroli lenye majani* na *mtu aliyesimama mbele ya malishio ya ng’ombe, na ng’ombe wakiwa wanakula.* Wanafunzi hawa walikosa uelewa kuwa toroli ni kifaa kinachotumika kubeba mizigo au mazao, kina magurudumu matatu au manne.

(c) Taja bidhaa mbili zinaweza kupatikana kwa mnyama anayeonekana katika picha hii.

(i) ____________________________________________

(ii) ____________________________________________

Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi kutambua bidhaa zinazoweza kupatikana kwa mnyama anayeonekana katika picha hii ambaye ni ng’ombe. Wanafunzi wenye uelewa walibaini kwa usahihi kwamba bidhaa zinazopatikana kutokana na ng’ombe ni pamoja na maziwa (yogati, siagi, jibini) na nyama (nyama ya ng’ombe) ambavyo ni vyakula bora na muhimu kwa afya ya binadamu. Pia ng’ombe hutupatia mbolea ya samadi ambayo hutumika kwenye masuala ya kilimo, ngozi ya ng’ombe (viatu, mikanda, mabegi), bidhaa zinazotokana na mifupa ya ng’ombe na mafuta ya ng’ombe.

Kwa upande mwingine, kuna wanafunzi walioandika majibu yasiyo sahihi, kama vile: *Ng’ombe anakula chakula*, *Ng’ombe anakula majani, Mtu, Jike Dume na Kuzalisha watoto.* Wanafunzi hawa hawakujua kuwa mtu ni kiumbe aliye na akili na uwezo wa kutembea kwa miguu miwili, mara nyingi hutumika kumaanisha binadamu. Jike ni mnyama wa kike katika muktadha wa wanyama wanaofugwa kama paka, mbwa, mbuzi, ng’ombe, nk. Dume ni mnyama wa kiume hasa katika muktadha wa wanyama wanaofugwa kama kondoo, ng’ombe, mbwa nk.


Wanafunzi wengine waliandika *kuzalisha watoto*; hawakujua kuwa ni hatua ya kuleta watoto duniani, mara nyingi huonesha tendo la uzazi. Kwa wale walioandika *anakula chakula,* hawakujua kuwa hiki ni kitendo cha kula ili kupata virutubisho vinavyohitajika mwilini. Aidha, wengine waliandika *anakula majani;* wanafunzi hawa hawakuelewa kuwa ni kitendo cha wanayama hasa wanaokula majani/mimea kama chanzo chao cha kujipatia chakula.

(d) Taja wanyama wengine wawili wanaofugwa nyumbani.

(i) ______________________________

(ii) ______________________________

Swali lilipima uwezo wa mwanafunzi kubainisha wanyama wengine wanaofugwa nyumbani. Wanafunzi wenye uelewa wa kutosha walitaja majibu sahihi ya wanyama wengine wanaofugwa nyumbani, kama vile *Mbuzi, Kondoo, Farasi, Punda, Paka, Mbwa, Nguruwe na Sungura.* Wanafunzi hawa walionekana kuwa na uelewa wa wanyama wafugwao na binadamu. Baadhi ya sifa za wanyama wanaofugwa nyumbani ni pamoja na: kuwa na tabia ya urafiki na upole, rahisi kufundishwa na kuzoea mazingira, wanahitaji matunzo maalumu, hawana tabia hatari kwa binadamu, wanahitaji nafasi ndogo za kukaa. Vilevile, walibaini faida za wanyama wanaofugwa nyumbani kuwa hutumika kwa ulinzi; kwa mfano, mnyama mbwa; kutoa maziwa, ngozi na sufi (mbuzi na kondoo); nyama na mbolea (nguruwe). Shughuli za kilimo, kuvuta na kubeba mizigo; usafiri; nyama; ngozi (Farasi). Wanyama kazi (kubeba mizigo, kuvuta magari; nyama; ngozi (punda)) pamoja na maziwa na nyama (mbuzi). Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 5.



**Maswali**

(a) Taja jina la wanyama waliopo kwenye picha: Ng'ombe

(b) Mtu anayeonekana katika picha anafanya nini? Anawalisha ng'ombe majani

(c) Taja bidhaa mbili zinazoweza kupatikana kwa mnyama anayeonekana katika picha hii.

(i) Maziwa

(ii) Nyama

(d) Taja wanyama wengine wawili wanaofugwa nyumbani.


(i) Mbuzi

(ii) Kondoo

**Kielelezo Na. 3.1:** *Sampuli ya Majibu Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 5*

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliandika majibu yasiyo sahihi, kama vile *Ng'ombe, Twiga, Simba.* Wanafunzi hawa hawakuwa na ufahamu kuwa ng'ombe hakuwa sehemu ya hitaji la swali. Pia, wanafunzi hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu wanyama wafugwao na binadamu, badala yake waliandika wanyama wasiofugwa na binadamu kama vile simba na twiga. Wanafunzi hawa walitakiwa kufahamu kuwa wanyama hao ni nyara za serikali. Twiga na simba ni wanyama pori ambao siyo sehemu ya wanyama wanaofugwa na binadamu. Hawakuelewa kuwa wanyama hawa wana maisha huru, wana mazingira maalumu, wana mifumo ya chakula (nyama/majani), wana tabia za kujilinda mfano; kukimbia kwa kasi, kujificha au kupigana, huzaliana katika mazingira ya asili na hupatikana kwa wingi katika maeneo maalumu. Wanyama hawa pia ni hatari kwa binadamu hususan simba ambaye ni mnyama anayekula nyama. Pia, inaonesha wanafunzi hawa hawakusoma kwa makini matakwa ya swali na hivyo kushindwa kujibu kwa usahihi. Kielelezo Na. 3.2

kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya wanafunzi kwa swali la 5.


**Maswali**

(a) Taja jina la wanyama waliopo kwenye picha. ngombe nyasi

(b) Mtu anayeonekana katika picha anafanya nini? nyasi ...

Kunywama majani Kama nyasi

(c) Taja bidhaa mbili zinazoweza kupatikana kwa mnyama anayeonekana katika picha hii.

(i) Ku ngombe Kulanyasi

(ii) maji wanyama wawili wanaofugwa nyumbani

(d) Taja wanyama wengine wawili wanaofugwa nyumbani.

(i) ngombe Kulanyasi

(ii) Kilofiku.


**Kielelezo Na. 3.2**: *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyosahihi katika swali la 5*

## 2.6 Swali la 6: Kuwa Mwadilifu

Swali hili lilitungwa kutoka katika Umahiri Mkuu *wa Kuwa mwadilifu,* na hususani kutoka umahiri mahususi wa *kutimiza majukumu yake kwa ukweli na uwazi.* Swali hili lilipima uwezo wa wanafunzi wa kubaini/kuelewa maudhui yaliyomo kwenye kifungu cha habari. Wanafunzi walitakiwa kusoma kifungu cha habari juu ya uadilifu wa wanafunzi, kisha kuandika majibu katika nafasi zilizoachwa wazi katika kipengele (a) hadi (d).

Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa kuwa wanafunzi 825,142 (53.91%) walipata alama 4 hadi 8. Uchambuzi

unaonesha kuwa wanafunzi 220,702 (14.42%) walipata alama 8, wanafunzi 302,377 (19.75%) walipata alama 6. Aidha, wanafunzi 302,063 (19.74%) walipata alama 4. Wakati wanafunzi wengine 705,370 (46.09%) hawakufanya vizuri kwa kuwa walipata alama kuanzia 0 hadi 2. Chati Na. 6 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 6.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa wanafunzi katika Swali la 6*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 6 ulifanyika kama ifuatavyo:

*Siku moja Mwalimu Mkuu alipita karibu na darasa letu na kusikia tukipiga kelele. Aliingia darasani na kutuamuru tutaje majina ya wanafunzi wote waliokuwa wakipiga kelele darasani, lakini sote tulikaa kimya na hatukutaja jina lolote. Mwalimu Mkuu aliasirika sana kwa sababu hatukutaja majina ya wanafunzi waliokuwa wakipiga kelele. Alisema kuwa sisi sio wawazi na waadilifu. Mwalimu mkuu alianza kutueleza tabia za mtu muwazi na mwadilifu. Alisema kwamba mtu muwazi na mwadilifu huwa hafichi maovu na hasemi uongo. Pia alisema kwamba mtu ambaye ni muwazi na mwadilifu hupata msaada kwa wakati anapohitaji kusaidiwa.*

*Baada ya hayo kiongozi wa darasa aliomba msamaha kwa niaba yetu. Aliahidi kusimamia nidhamu ya darasa na kuandika majina ya wanafunzi wote watakaopiga kelele. Mwalimu Mkuu alifurahi na kuondoka. Nasi kwa upande wetu, tuliweka nia ya dhati ya kuwa wawazi na waadilifu.*

**Maswali:**

(a) Mwalimu mkuu aliwezaje kusikia wanafunzi walipokua wakipiga kelele?

____________________________________________

Swali hili lilipima uwezo wa wanafunzi kutambua njia mtu anayoweza kutumia ili kusikia kelele kutoka darasani. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi umebaini kuwa wanafunzi waliokuwa na ujuzi wa kuelewa kifungu cha habari waliandika jibu sahihi *Kwa Sababu alipita karibu na darasa.* Wanafunzi hawa walielewa kuwa uhakika wa kubaini kilichokuwa kinaendelea darasani ni kuona au kuwemo katika darasa, au kupita karibu na darasa. Mwalimu Mkuu kupita karibu na darasa kulimwezesha kusikia wanafunzi waliokuwa wanapiga kelele darasani.

Kwa upande mwingine, wanafunzi ambao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya kufahamu maudhui kutoka katika kifungu cha habari waliandika majibu yasiyo sahihi, kama vile *kutopiga kelele, kutokuwaheshimu na wazazi, msipige kelele, alipita dirishani*. Majibu yasiyokuwa sahihi yalidhihirisha wanafunzi hawakuwa na maarifa juu ya uelewa wa kifungu cha habari. Aidha, wanafunzi hawa walikosa umakini na hawakuwa na misingi ya kufahamu kwa ufasaha lugha ya Kiswahili.

(b) Ni tabia zipi mbili za mtu muwazi na mwadilifu zilizotajwa na Mwalimu mkuu?

(i) ________________________________________

(ii) ________________________________________

Swali hili lilipima uwezo wa mwanafunzi kuelewa na kubaini tabia za mtu muwazi na mwadilifu. Wanafunzi waliosoma kifungu cha habari kwa umakini walibainisha kwa usahihi tabia za mtu muwazi na mwadilifu kuwa ni *hafichi maovu na hasemi uongo.* Wanafunzi hawa walielewa kuwa uadilifu ni maadili thabiti ya kufanya mambo kwa njia ya haki hata pale ambapo hakuna mtu anayekuona. Pia, ni kuishi kulingana na misingi ya ukweli, haki na uaminifu bila upendeleo. Uwazi ni kuweka taarifa wazi, kushirikiana na wengine katika maamuzi na kutenda kwa njia isiyo na usiri. Baadhi ya sifa za uwazi na uadilifu ni pamoja na kutoficha maovu au kutosema uongo, kujenga imani na uaminifu, kukuza ushirikiano na amani, kuimarisha maendeleo, kuongeza uwajibikaji, kuimarisha ufanisi, na kuleta maadili mema katika jamii. Kwa ujumla, uwazi na uadilifu ni nguzo muhimu za kujenga jamii iliyo imara yenye haki kwa kila mmoja.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi umeonesha kuwepo kwa wanafunzi ambao hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu ufahamu (kifungu cha habari). Walishindwa kuandika maneno sahihi, kisha kuandika majibu yasiyo sahihi kama vile: *kuandika, tusipige kelele, kupiga kelele, husaidiwa haraka, muwazi, mwadilifu na kukataza kelele darasani*. Wanafunzi hawa hawakujua kuwa kuandika ni kitendo cha kuweka maandishi kwa kutumia kalamu, penseli, kompyuta n.k, kinachoweza kuwasilisha mawazo, taarifa au ujumbe kwenye karatasi. Kupiga kelele ni kitendo cha kutoa sauti kubwa na ya juu kwa nia ya kuvuta hisia, furaha, au kutafuta msaada. Pia, kusaidiwa haraka ni hali ya kupokea msaada kwa muda mfupi bila kuchelewa, hasa pale ambapo kuna dharura ya kutatuliwa. Wanafunzi hawa hawakuwa na uelewa kuwa mtu muwazi na mwadilifu ni mtu mkweli, mwaminifu na mwenye matendo mazuri.

(c) Kutokana na habari uliyosoma, nini faida ya kuwa mwadilifu na muwazi?

____________________________________________________________

____________________________________________________________


____________________________________________________________

Swali hili lilipima uwezo wa mwanafunzi kutathmini faida za kuwa mwadilifu na muwazi. Wanafunzi waliokuwa na maarifa na uwezo wa kusoma kifungu cha habari kwa umakini na kuelewa waliandika majibu sahihi ambayo ni *hupata msaada kwa wakati anapohitaji kusaidiwa* au *kupata msaada pindi anapohitaji* au *kupewa msaada wa haraka.* Wanafunzi hawa walikuwa na uelewa kuwa mtu muwazi na mwadilifu hupendwa na jamii kwa sababu ya tabia zake nzuri, na hata anapopata changamoto ya aina yoyote wanajamii wapo tayari kumsaidia kutatua changamoto hiyo. Faida nyingine za kuwa mwadilifu na muwazi ni pamoja na kuaminika na kujenga uhusiano imara, utulivu wa moyo na akili, kujenga sifa nzuri, kuaminika katika jamii, kufanya maamuzi sahihi, kuimarisha maadili na nidhamu. Kwa ujumla, kuwa mtu mwadilifu na muwazi husaidia kuboresha maisha binafsi, mahusiano, na jamii kwa ujumla. Ni misingi ya kuishi maisha yenye heshima, furaha, na mafanikio. Wanafunzi hawa walitambua kuwa mtu muwazi na mwadilifu huwa na marafiki wengi na wenye tabia nzuri. Kwa upande mwingine, mtu ambaye siyo muwazi na mwadilifu, kutokana na tabia zake anaweza kuleta ugomvi, chuki, uvunjifu wa amani na kutoaminika katika jamii.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi waliandika majibu yasiyo sahihi kutokana na kutokuwa na maarifa na ujuzi wa kusoma na kuelewa kifungu cha habari. Wanafunzi hao waliandika majibu yasiyo sahihi kama vile: *kuwa na tabia njema, usidanganye mtu, utapendwa na jamii, kwa sababu usipokua mkweli, utakua mtoto muongo.* Wanafunzi hawa walikosa maarifa juu ya faida za mtu kuwa muwazi na mwadilifu na kuandika majibu yasiyoendana na matakwa ya swali na maelezo yaliyopo kwenye kifungu cha habari.

(d) Kwa nini Mwalimu Mkuu aliondoka kwa furaha?

Swali hili lilipima matarajio ya kitendo cha mwalimu mkuu kuondoka darasani kwa furaha. Wanafunzi waliosoma kifungu cha habari kwa umakini na kuelewa waliandika kuwa jibu sahihi ni *kwa sababu kiongozi wa darasa aliomba msamaha kwa niaba ya wanafunzi na kuahidi kusimamia nidhamu ya darasa na kuandika majina ya wote watakaopiga kelele*. Wanafunzi hawa walikuwa na uelewa kuwa mtu anapofanya kosa ni vizuri kuomba msamaha na kuahidi kutokurudia kosa. Walijua kuwa mtu anapofanya kosa anatakiwa kukubali kosa, kuomba msamaha, kujifunza kutokana na makosa, kutafuta ushauri na kuboresha tabia, na kuchukua tahadhari. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi kwa swali la 6.


**Maswali**

(a) Mwalimu Mkuu aliwezaje kusikia wanafunzi walipokuwa wakipiga kelele?
Alipita karibu na darasa

(b) Ni tabia zipi mbili za mtu muwazi na mwadilifu zilizotajwa na Mwalimu Mkuu?
(i) Kutoficha maovu
(ii) Kutosema uongo


(c) Kutokana na habari uliyosoma, nini faida ya kuwa mwadilifu na muwazi?
Anapata msaada kwa haraka

(d) Kwa nini Mwalimu Mkuu aliondoka kwa furaha?
Kiongozi wa darasa aliomba msamaha

**Kielelezo Na. 4.1:** *Sampuli ya Majibu Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 6*

Wanafunzi wengine waliokosa maarifa ya kusoma na kuelewa kifungu cha habari, hivyo waliandika majibu yasiyo sahihi kama

vile: *nasi kwa upande wetu tuliweka nia ya dhati, kwa sababu kiranja alimjibu vizuri.* Baadhi ya wanafunzi waliandika maneno yasiyoeleweka; kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika: *mais, matimyi, shidais, zaimtu na maish*. Wengine waliandika maneno yaliyounganishwa, hivyo kutoeleweka mantiki yake. Mfano. Mwanafunzi mmoja aliandika: *zipimbiizemtuyamakanaga, bemagokananauawanaya* na *mimimabangamakaneyanga*. Majibu yote haya yanaonesha kuwa wanafunzi hawakujua walichokuwa wanatakiwa kuandika, na kwamba hawakuwa na maarifa yanayohusiana na kusoma na kuelewa kifungu cha habari. Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika Swali la 6.



**Maswali**

(a) Mwalimu Mkuu aliwezaje kusikia wanafunzi walipokuwa wakipiga kelele?
Aliambiwa na Kiongozi wa darasa

(b) Ni tabia zipi mbili za mtu muwazi na mwadilifu zilizotajwa na Mwalimu Mkuu?
(i) Anajua michoro mingi
(ii) Ana akili nyingi sana

(c) Kutokana na habari uliyosoma, nini faida ya kuwa mwadilifu na muwazi?
Kupata marafiki wengi na zawadi nyingi

(d) Kwa nini Mwalimu Mkuu aliondoka kwa furaha?
Aliambiwa ukweli mtupu

***Kielelezo Na. 4.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 6*

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI

Uchambuzi wa umahiri katika maswali ya upimaji wa kitaifa wa Darasa la Nne kwa somo la Uraia na Maadili unaonesha kuwa kati ya aina tano (5) za umahiri uliopimwa, wanafunzi walifanya vizuri zaidi kwenye umahiri wa *Kuwa Mwajibikaji* (83.86%) swali la 5, *Kuwa Mstahimilivu* (74.17%), uliopimwa kwenye swali la 3 na *Kuheshimu Jamii* (69. 67%) kwenye swali la 2 na la 4. Aidha, umahiri wa *Kudumisha Amani (56.70%) katika swali la 1 na umahiri wa Kuwa Mwadilifu (53.91%) swali la 6, ulikuwa na ufaulu wa wastani.*

Vilevile, ulinganifu wa ufaulu wa umahiri kati ya upimaji wa kitaifa wa Darasa la Nne kwa mwaka 2024 na 2023 unaonesha kuwa kiwango cha ufaulu cha umahiri wa *Kuwa Mwajibikaji umekuwa mzuri (83.86%)* kwa mwaka 2024 sawa na mwaka 2023 ambapo ulikuwa asilimia 74.27. Viwango vinafanana japokuwa kuna ongezeko la asilimia ya ufaulu kwa mwaka 2024, ambao ni asilimia 9.59. Ufaulu katika umahiri wa *Kuwa Mstahimilivu* una kiwango kizuri cha asilimia 74.71 kwa mwaka 2024, ambapo mwaka 2023 umahiri huo haukupimwa. Ufaulu wa umahiri wa *Kuheshimu Jamii* kwa mwaka 2024 umeongezeka kutoka kiwango kizuri cha wastani wa asilimia 69.67 kwa mwaka 2024; ambapo mwaka 2023 umahiri huo ulikuwa na ufaulu hafifu wa asilimia 20.31. Umahiri wa *Kudumisha Amani* umeendelea kuwa wa kiwango cha wastani kwa asilimia 56.70 katika mwaka 2024 na asilimia 48.58 katika mwaka 2023.

Pia, umahiri wa *Kuwa Mwadilifu* kiwango cha ufaulu kimepungua kwa kuwa na asilimia 53.91 katika mwaka 2024, ambapo mwaka 2023 ulikuwa asilimia 81.71. Ufaulu huo umepungua kwa asilimia 27.80. Halikadhalika, umahiri wa *Kuithamini Jamii* haukupimwa mwaka 2024, wakati mwaka 2023 ulipimwa na kuwa na maswali mawili: swali la 3 (69.35%) na swali la 5 (43.62%). Hali kama hiyo imeonekana katika upimaji wa 2024, ambapo umahiri wa

*Kuheshimu Jamii* ulikuwa na maswali mawili: swali la 2 (74.17%) na swali la 4 (65.16%).

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Uraia na Maadili umeonesha kuwa, kwa ujumla, wanafunzi wamefaulu kwa kiwango kizuri. Wanafunzi waliopata Daraja A hadi D walikuwa asilimia 86.35. Aidha, wanafunzi wachache ambao ni asilimia 13.65 walipata kiwango hafifu cha ufaulu wa Daraja E. Wanafunzi waliofanya vizuri katika upimaji huu walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika aina za umahiri uliopimwa. Aidha, wanafunzi hao walibaini matakwa ya maswali.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi umebaini changamoto mbalimbali walizokuwa nazo wanafunzi, na hivyo kuwa na ufaulu hafifu. Baadhi ya changamoto hizo ni kutokuwa na maarifa ya kutosha katika aina za umahiri uliopimwa, kushindwa kuelewa matakwa ya swali, na hivyo kushindwa kuandika majibu sahihi. Vilevile, wanafunzi walionesha ukosefu wa umahiri katika maswali ya stadi za kutafsiri picha na kifungu cha habari katika swali la 5 na 6, mtawalia.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha ufaulu kwenye somo la Uraia na Maadili, Baraza la Mitihani linapendekeza mambo yafuatayo:

(a) Wanafunzi wapewe kazi za nyumbani na kazi za vikundi ili kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anakuwa na umahiri unaotakiwa, hasa katika umahiri wa *Kudumisha Amani* na Kuwa *Mwadilifu* ambao umebainika kuwa na changamoto. Kazi hizo zisahihishwe na mrejesho utolewe kwa wanafunzi.

(b) Walimu waweke msisitizo wa kusoma na kuandika ili kujenga msingi mzuri kwa wanafunzi wa madarasa husika. Kwa kuwa baadhi ya wanafunzi wanakosa umahiri huo.

(c) Walimu wanashauriwa kutumia zaidi mbinu shirikishi, kama vile igizo dhima, majadiliano ya kikundi, maswali na majibu, michezo ya kuelimisha na kazi mradi hususan katika umahiri wa *Kudumisha Amani* na *Kuwa Mwadilifu*. Mbinu hizi huwezesha ushiriki wa wanafunzi, huimarisha uelewa, hujenga uwezo wa kufikiri na kutatua matatizo na hufanya ujifunzaji kuvutia zaidi.

(d) Walimu watunge maswali yenye kupima umahiri ili yatumike na wanafunzi katika ngazi ya shule; yanaweza kutumika katika upimaji katikati ya mihula, au mwisho wa mihula. Maswali hayo yaakisi maswali yanayotumika katika ngazi ya Upimaji wa Kitaifa. Maswali haya yatachochea uwezo wa kufikiri kwa kina, kuibua maarifa mapya na kujenga fikra tunduwizi.

(e) Walimu washirikiane na wazazi katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wanasoma vitabu mbalimbali vya kiada na ziada ili kuimarisha uelewa wa umahiri wa somo la Uraia na Maadili, hususan katika umahiri wa *Kudumisha Amani* na *Kuwa Mwadilifu*.

*Kiambatisho*

Ulinganifu wa ufaulu kwa wanafunzi katika kila umahiri kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na mwaka 2023

| **Na.** | **Umahiri** | **Upimaji 2024** | | | | **Upimaji 2023** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Ufaulu wa kila swali** | | **Wastani wa ufaulu (%)** | **Maoni** | **Ufaulu wa kila swali** | | **Wastani wa ufaulu (%)** | **Maoni** |
| | | **Namba ya swali** | **(%) wastani wa ufaulu** | | | **Namba ya swali** | **(%) wastani wa ufaulu** | | |
| 1 | Kuwa Mwajibikaji | 5 | 83.86 | 83.86 | Vizuri | 4 | 74.27 | 74.27 | Vizuri |
| 2 | Kuwa Mstahimilivu | 3 | 74.71 | 74.71 | Vizuri | | | | |
| 3 | Kuheshimu Jamii | 2 | 74.17 | 69.67 | Vizuri | 2 | 20.31 | 20.31 | Hafifu |
| | | 4 | 65.16 | | | | | | |
| 4 | Kuithamini Jamii | | | | | 3 | 69.35 | 56.48 | Wastani |
| | | | | | | 5 | 43.62 | | |
| 5 | Kudumisha Amani | 1 | 56.70 | 56.70 | Wastani | 6 | 48.58 | 48.58 | Wastani |
| 6 | Kuwa Mwadilifu | 6 | 53.91 | 53.91 | Wastani | 1 | 81.71 | 81.71 | Vizuri |